JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

# UGAWAJI WA MASAFA YA BENDI 3600-3800 MHz KWA NJIA YA USHINDANI

Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imepewa jukumu la kupanga, kuidhinisha, kugawa, kutoa, kuchukua, kusimamisha matumizi, kufuta au kwa namna yoyote ile kurekebisha mgawo wa masafa miongoni mwa watumiaji au wenye leseni za masafa ya mawasiliano.

Katika kutekeleza majukumu yake, TCRA pia inaongozwa na Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 ambayo malengo yake makuu kuhusu matumizi ya masafa ya mawasiliano ni:

i) Kukuza ufanisi katika matumizi ya masafa (ambapo ufanisi unamaanisha kutoa masafa kwa wale ambao watatumia masafa na kuleta manufaa makubwa zaidi ya kiuchumi na kijami);

ii) Kukuza ushindani, ili kuleta matokeo yatakayochochea na yasiyofifisha ushindani wenye tija;

iii) Kukuza manufaa kwa watumiaji, kupitia utoaji endelevu wa huduma zenye ubora wa juu na zilizoenea; na

iv) Kukuza uwekezaji na ubunifu.

Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016, na kufuatia maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Usimamizi wa Masafa Duniani wa mwaka 2023 (WRC-23) chini ya uratibu wa Shirika la Kimataifa la Mawasiliano Duniani (ITU), TCRA imepanga kugawa masafa katika bendi ya 3600-3800 MHz kwa ajili ya mawasiliano ya simu na intaneti, ambapo yataleta manufaa mbalimbali kwa Taifa, yakiwemo: -

a) Kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ya simu na intaneti (broadband) ambayo itachochea maendeleo ya uchumi wa Taifa, hususan uchumi wa kidijiti, ili kuwezesha ukuaji wa sekta zote;

b) Uwezeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye utoaji wa huduma kama vile elimu, afya, kilimo, biashara, huduma za kifedha kupitia TEHAMA;

c) Kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji;
d) Kupanua utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kwa Watanzania wengi zaidi; na
e) Kukuza, kuimarisha na kuwezesha ubunifu wa huduma mpya za TEHAMA na matumizi yake.

TCRA inapenda kuufahamisha Umma na wadau kwa ujumla kwamba imepanga kugawa masafa ya 3600-3800 MHz katika vitalu vinne (4) vya 1 x 50 MHz vilivyotengwa kwa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kwa njia ya ushindani. Katika kuhakikisha kuwa watumiaji wananufaika kikamilifu na huduma za Mawasiliano ya simu na intaneti, TCRA itaweka masharti ya usambazaji na utoaji wa huduma kwa matumizi ya masafa husika.

Ratiba ya awali imetolewa katika tangazo hili ili kuwapa wadau nafasi ya kuweka mipango ya awali kwa ajili ya mnada wa masafa uliopangwa.

**Ratiba ya awali**

| Na. | TUKIO | MUDA |
|---|---|---|
| **1** | Taarifa kwa Umma - Rasimu ya Waraka wa taarifa ya Ugawaji wa Masafa kwa njia ya ushindani (Publication of Consultation Document - Draft Information Memorandum) | Februari 2025 |
| **2** | Kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu ya Waraka wa Taarifa ya Ugawaji wa Masafa kwa njia ya ushindani | Aprili 2025 |
| **3** | Kutoa majibu ya maswali, maoni na ushauri wa wadau | Mei 2025 |
| **4** | Taarifa kwa Umma - Waraka wa taarifa ya Ugawaji wa Masafa kwa njia ya ushindani (Publication of Information Memorandum) | Juni 2025 |
| **5** | Kufanyika kwa Mnada wa Masafa | Julai 2025 |

Imetolewa Tarehe **18 Desemba, 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**